

## **Mwelekeo wa Usarufishaji wa Nomino za Kiswahili zenye Asili ya Kiingereza na Kiarabu**

*Johari Hakimu<sup>1</sup>*

### **Ikisiri**

Makala hii inaonesha mwelekeo wa usarufishaji wa nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Mwelekeo wa nomimo hizo umeoneshwa kwa kutumia data iliyokusanywa kwa njia ya upitiaji wa nyaraka. Nyaraka zilizopitiwa ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2022) na *Kamusi ya Karne ya 21* (2021). Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kutumia Nadharia ya Mofolojia ya Ongezeko la Maneno na kufafanuliwa kwa kutumia Nadharia ya Usarufishaji. Uchanganuzi na ufafanuzi wa data hizo umeonesha kuwa kuna mielekeo chanya na hasi ya usarufishaji wa nomino za Kiswahili kwa kuzingatia ngeli za majina. Mwelekeo chanya wa usarufishaji wa nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu umeonesha mchakato wa usarufishaji uliokamilika katika Kiswahili. Mwelekeo hasi umedhihirisha usarufishaji usiokamilika katika baadhi ya nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Kwa ujumla, ufafanuzi wa nomino za Kiswahili unapaswa kuzingatia mazingira ya namna zinavyojitokeza na kusarufishwa katika lugha hii.

### **1.0 Utangulizi**

Neno ‘mwelekeo’ limetumika katika makala hii kwa maana ya mabadiliko yanavyojitokeza katika maneno ya lugha kwa kufuata upande maalumu ambao matumizi ya maneno yanaelekea. Upande unaokusudiwa unaweza kuwa mmojawapo kati ya pande mbili ambazo ni mwelekeo chanya au hasi. Mwelekeo chanya unaonesha mabadiliko ya maneno kwa kufuata taratibu msingi za lugha. Vilevile, mwelekeo hasi unaonesha mabadiliko ya maneno yasiyofuata taratibu msingi za lugha. Kwa hiyo, mwelekeo wa usarufishaji wa nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu umeshughulikiwa katika makala hii kwa kuzingatia mielekeo chanya na hasi ya nomino hizo ili kuweka wazi upande unaofuatwa kwa namna zilivyosarufishwa katika Kiswahili. Uwekaji wazi wa mielekeo hiyo ni muhimu kwa sababu lugha ya Kiswahili ina maneno mengi yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu (Mwaliwa, 2018; Dzahene-Quarshie, 2010). Hivyo, ni muhimu kuonesha namna yanavyotumika katika Kiswahili. Uthibitisho

---

<sup>1</sup> Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania. Barua pepe: [jhakimu@mzumbe.ac.tz](mailto:jhakimu@mzumbe.ac.tz)

wa Kiswahili kuwa na maneno mengi ya Kiingereza na Kiarabu kuliko lugha zingine za kigeni kama: Kijerumani, Kifaransa, Kireno na Kiajemi umetokana na etimolojia za maneno zilizobainishwa katika kamusi za Kiswahili (TATAKI, 2013; TUKI, 2014; BAKITA, 2022). Mifano ya maneno ya Kiswahili yenye asili za kigeni ni kama: *chenji, kompyuta* (Kiingereza); *gharika, amani* (Kiarabu); *shule* (Kijerumani), na *bahasha, bandari* (Kiajemi) (TUKI, 2014). Maneno hayo ya kigeni hukopwa kutoka lugha moja kwenda nyingine kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwazo ni: mosi, uhitaji wa neno jipya la kutaja kitu au mnyama kutokana na mwingiliano wa watu, lugha na tamaduni mbalimbali. Kukosekana kwa msamiati wa kutaja jambo miongoni mwa hayo, huweza kuwa sababu ya ukopaji. Pili, utambulisho kutokana na utumiaji wa maneno ya kigeni. Mtumiaji wa maneno hayo hudhani kuwa kwa kutumia maneno ya kigeni atakuwa amejitambulisha hali yake kama hadhi, elimu, asili, n.k. Tatu, uchanganyaji msimbo hufanya baadhi ya maneno ya lugha ya kigeni kuzoeleka na kuendelea kutumika hasa kwa watumiaji wenye lugha ulumbi. Nne, baadhi ya watu hutumia maneno ya kigeni kama njia ya kujifaharisha au kujipandisha hadhi na kujinasibisha na maneno ya kisasa kutoka lugha inayodhaniwa kuwa ni yenye hadhi ya juu kuliko lugha yao ya kwanza (Katamba, 1994; Egbe na Akpan, 2016; Panhwar na wenzake, 2021). Sababu hizi zinaashiria kuwa ukopaji katika lugha mbalimbali hufanyika ukiwa na sababu tofautitofauti.

Pamoja na kwamba Kiswahili kimekopa maneno kutoka lugha mbalimbali na kwa sababu mbalimbali, makala hii imeshughulika na maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Hii ni kwa sababu Kiswahili kina utangamano mkubwa na lugha hizi mbili. Awali kabisa, Kiswahili kilitangamana na Kiarabu katika kipindi cha ujio wa Waarabu katika pwani ya Afrika Mashariki (Massamba, 2015). Utangamano huo ukawa sababu ya lugha hiyo kuwa na maneno mengi ya Kiarabu. Pia, ukaribu wa Pwani ya Afrika Mashariki na ghuba ya Uarabuni unaelezwa kuwa sababu mojawapo ya lugha hii kuwa na maneno mengi ya Kiarabu (Mwaliwa, 2018). Kwa upande mwingine, Kiswahili kimetangamana zaidi na Kiingereza. Hii inatokana na sababu kwamba Kiswahili na lugha nyingine za Kirafrica zimetagusana na lugha ya Kiingereza tangu enzi za ukoloni wa Waingereza (Dzahene-Quarshie, 2010). Vilevile, lugha ya Kiingereza imetagusana zaidi na lugha ya Kiswahili kutokana na nafasi yake na matumizi ya lugha hiyo katika nchi za Afrika Mashariki. Katika Tanzania kwa mfano, Kiingereza kina nafasi na hadhi ya juu kwa sababu ni lugha ya kufundishia katika ngazi kadhaa za elimu na inatumika kama lugha rasmi katika maeneo muhimu yaliyoidhinishwa na serikali. Vilevile, lugha ya Kiingereza ni ya kwanza kimataifa na yenye nguvu. Pia, ina ushawishi na athari kubwa kwa lugha nyingi ulimwenguni kwa sababu ni lugha ya mwingiliano wa mataifa na biashara (Dzahene-Quarshie, 2010; Ideh na Tibetegeza 2022). Kwa hiyo, mazingira yanayoukilia mtagusano wa lugha ya Kiswahili na lugha hizi (Kiarabu na

Kiingereza) yamechochea kuchunguza mwelekeo wa usarufishaji wa nomino za Kiswahili zenye asili ya lugha hizo.

Pamoja na kwamba lugha ya Kiswahili ina aina mbalimbali za maneno ya lugha ya Kiarabu na Kiingereza, nomino ndizo zilizohusishwa katika makala hii. Hii inatokana na sababu inayoelezwa na Katamba (1994) kwamba katika uhalisi maneno yanayokopwa zaidi ni nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi. Pia, Katamba anaongeza kuwa katika aina hizo za maneno, nomino zinakopwa zaidi zikifuatiwa na vitenzi na vivumishi. Sababu ya nomino kukopwa zaidi sio ngumu kuiona kwa sababu mara nyingi lugha hukopa neno jipya kwa ajili ya kutaja vitu mbalimbali visivyofahamika (Katamba, 1994).

Ingawa kuna wataalamu mbalimbali (Polome, 1967; Schadeberg, 2001; Dzahene-Quarshie, 2012; Mgullu, 2012; Mdee, 2014) walioshughulikia nomino za Kiswahili na za kigeni, suala la mwelekeo wa usarufishaji wa nomino za kigeni haliko wazi kimofolojia na kisintaksia. Hii ina maana kwamba uchambuzi wa nomino za Kiswahili hauoneshi wazi iwapo nomino za kigeni zinasambaa katika kila ngeli za majina kiukamilifu au la. Pia, uchambuzi hauoneshi iwapo nomino hizo zina sifa sawa na nomino zinazolingia katika ngeli husika na kama zinabeba viambishi vya ngeli sawa na nomino nyingine za Kiswahili asilia. Hata hivyo, baadhi ya wataalamu wameonesha kuwa baadhi ya nomino za kigeni zinaangukia katika ngeli isiyokuwa na viambishi vya umoja na wingi {N-/N-}, lakini baadhi ya nomino za Kiswahili asilia huanza na sauti za nazali kama /n/ *nyota*, /m/ *mbolea*, /ŋ/ *nguo* na /j/ *nyuzi*. Kwa mfano, Mdee (2014: 40) anaonesha kuwa nomino za ngeli hiyo ambayo ni ya 9/10 katika umoja na wingi mtawalia inaitwa ngeli ya N kwa kuwa nomino zake huanza na nazali isipokuwa nomino za kigeni ambazo hazina viambishi vya umoja wala wingi. Kwa hiyo, kutokana na baadhi ya nomino za kigeni kuwa na tabia tofauti na zile za Kiswahili asilia, bado ufafanuzi unahitajika kwa kuzingatia ngeli za nomino za Kiswahili kwa ujumla. Ufafanuzi huo unahitajika kwa ajili ya kuonesha mwelekeo wa usarufishaji wa nomino hizo ili kuwa na namna moja ya kuzieleza hasa katika taaluma za mofolojia na sintaksia.

## 2.0 Dhana Usarufishaji

Dhana ya usarufishaji imefasiliwa kwa namna tofauti na wataalamu mbalimbali wa lugha. Katika makala hii tumezigawa fasili hizo katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusu fasili ya usarufishaji mahususi na kundi la pili linahusu usarufishaji wa jumla. Kundi la kwanza linafasili dhana ya usarufishaji kama utaratibu wa kubadili mofimu huru yenye maana ya kisemantiki na kuifanya mofimu funge yenye maana ya kisarufi (Massamba, 2004; Gichuru, 2020). Katika fasili hii, mofimu imechukuliwa kuwa ni umbo ambalo kiuhalisi ndilo mofu. Fasili hii imesemwa kuwa mahususi kwa sababu imejegemeza upande wa mofolojia kama uwanja maalumu wa kitaaluma kwa kuwa inahusu mabadiliko ya mofimu huru. Usarufishaji huu unahusisha neno lililoambikwa kiambishi chochote cha

kisarufi na ambalo halijaambikwa. Hivyo, uambikaji wa viambishi mbalimbali vya kisarufi katika neno huonesha mchakato wa usarufishaji unavyofanyika.

Vilevile, fasili hii imechukuliwa kuwa mahususi kwa sababu mofimu huru (kwa maana ya umbo au mofu huru) ni ile inayoweza kusimama peke yake na ikajitosheleza kimaana, kama vile *pombe*, *kalamu*, *pua*, n.k. (Massamba, 2004). Kutokana na fasili hii, inawezekanaje mofu huru inayojitegemea ikaweza kuambikwa? Kutokana na swali hili, tunaona kuwa kinachomaanishwa si mofu huru bali neno au shina la neno ambalo halijaambikwa viambishi vyovyote vya kisarufi. Neno hilo linaweza kuwa katika muundo wa kidahizo kinachoingizwa kwenye kamusi na kutolewa maana. Kwa hali hii, fasili iliyotolewa na Geurts (2000) kuwa usarufishaji ni ule unaohusu mchakato wa mabadiliko ya lugha ambapo umbo la neno linatoka katika hali ya kuwa leksimu na kuwa neno la kisarufi, ndiyo imekidhi zaidi maana ya dhana hii tofauti na ya Massamba (2004) na Gichuru (2020). Pia, hii inaweza kuelezwa kuwa inahusu neno lenye mzizi tegemezi unaoambishika. Kwa ujumla, neno hili likiambikwa viambishi mbalimbali vya kisarufi linakuwa limesarufishwa.

Kundi la pili linafasili usarufishaji kuwa ni utaratibu unaoliathiri neno katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki (Gichuru, 2020) na sio mofolojia na maana peke yake kama ilivyo kwa fasili yenye umahususi. Kwa maana hii, neno la Kiswahili lenye asili ya kigeni likiwa katika hali ya leksimu linaweza kuchunguzwa usarufishwaji wake kwa kuzingatia viwango vyote vya kisarufi. Kwa hiyo, kwa kuwa makala hii inahusisha ngeli za majina kwa kuzingatia viambishi vyake ya umoja na wingi na upatanisho wake katika tungo, fasili zote mbili zimekuwa muhimu kuzingatiwa. Hii ni kwa sababu nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu zimeangaliwa iwapo zinapokea viambishi vya umoja na wingi vya ngeli za majina na vya upatanisho wa kisarufi (zitumikapo katika sentensi) sawa na ilivyo kwa nomino za Kiswahili asilia. Vilevile, iwapo msambao wa nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu uko sawa na nomino za Kiswahili asilia katika mpangilio wa ngeli za nomino. Hivyo, upokeaji wa viambishi vya umoja na wingi, msambao wa nomino hizo katika ngeli hizo za majina, na upatanisho wake wa kisarufi umetusaidia kuutambua usarufishaji wenye mwelekeo chanya (ulikokamilika) au hasi (usiokamilika) kwa mujibu wa Nadharia ya Usarufishaji.

### 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa kwa njia ya upitiaji wa nyaraka. Nyaraka zilizopitiwa ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (toleo la 3) na *Kamusi ya Karne ya 21* (toleo la 4). Kamusi hizi zimeteuliwa kwa sababu ndizo kamusi za Kiswahili zenye matoleo ya hivi karibuni zaidi (2022 na 2021). Lengo la kuhusisha kamusi hizi ni kupata maneno mengi na mapya zaidi. Vilevile, kamusi hizo zilihusishwa ili kuona usahihi wa asili za maneno yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu yaliyohusishwa katika makala hii kwa sababu ya kuwapo kwa etimolojia ya maneno ya kigeni

katika kamusi hizo. Kwa hiyo, vidahizo vya nomino kutoka kamusi hizo vilikusanywa kwa kuzingatia taarifa zake za kisarufi kama viambishi vyake vya umoja au wingi na vile vya upatanisho wa kisarufi ili kutambua nomino huru (ambazo hazina viambishi vya umoja wala wingi) na tegemezi (zinazobeba viambishi). Uchanganuzi wa data iliyokusanywa ulitumia Nadharia ya Ongezeko la Maneno ili kuonesha mipaka ya viambishi mbalimbali vilivyoambikwa katika maneno ya kigeni kwa kuzingatia mgawanyo wa viambishi vya ngeli vilivyobainishwa na Mgullu (2012). Hivyo, maneno ya kigeni yamechunguzwa yakiwa na viambishi hivyo ili kuona tabia zake na hatimaye kuona mwelekeo wa usarufishaji wake. Sambamba na Nadharia ya Ongezeko la Maneno, Nadharia ya Usarufishaji ilitumika kwa azma ya kufafanua data iliyochanganuliwa ili kuonesha mwelekeo wa usarufishaji wa nomino hizo.

#### **4.0 Nadharia Zilizotumika katika Uchanganuzi wa Ufafanuzi wa Data**

Makala hii imetumia nadharia mbili katika uchanganuzi na ufafanuzi wa data. Nadharia ya kwanza ni ya Ongezeko la Maneno. Kwa mujibu wa Stump (2001) nadharia hii iliasisiwa na Lieber (1992). Nadharia hii inahusu mofolojia ya uambishaji ambapo inaelezwa kuwa mofolojia ya namna hii ni ya uongezaji taarifa. Taarifa zinazoongezwa ni za viambishi vyenye dhima mbalimbali. Kwamba neno linapata sifa za kimofosintakisia kama kiambata pekee cha kujipatia viambishi wakilishi vya sifa hizo. Katika nadharia hii inaelezwa kuwa uambikaji wa viambishi una mipaka maalumu. Kila kiambishi kina nafasi yake ambayo inaweza isikaliwe na kiambishi kingine. Katika lugha ya Kiingereza, kwa mfano, kiambishi *-s* cha wakati kinatokea katika vitenzi tu na sio katika aina nyingine ya neno. Hivyo, kiambishi kinaungana na shina la kitenzi na sifa nyingine za kimofosintakisia katika neno zima kwa mbinu ya kupenyeza au kupachika viambishi vyenye sifa za kisintakisia katika mizizi yake. Mfano unaotolewa hapa ni neno la Kiingereza *likes* ambalo linapata viambishi vya kisintakisia ambapo viambishi vya upatanisho vya wakati vinaweza kupachikwa na kuonesha hali ya kuarifu katika shina lake, yaani *like*. Pia, kiambishi kimoja kina uwezo wa kufanya kazi zaidi ya moja katika shina la kitenzi. Kwa mfano, katika sentensi ya Kiingereza *Juma likes ugali*, yaani 'Juma hupenda ugali'. Ina maana kwamba {-s} ya kwenye *likes* inafanya kazi ya upatanisho wa njeo na hali ya kuarifu. Kama ilivyo kwa kiambishi {hu-} kwenye kitenzi cha Kiswahili *hupenda*, baada ya kutafsiriwa {hu-} imefanya kazi ya njeo timilifu, kuarifu na nafsi ya pili. Kwa hiyo, nadharia hii imetumika kwa kuwa inahusisha mipaka ya viambishi. Nafasi ya viambishi vya ngeli katika nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu ambayo ni kabla ya mzizi wa nomino imeoneshwa. Hii inaonesha iwapo nomino za Kiswahili zenye asili y Kiingereza na Kiarabu zinabeba viambishi vya ngeli katika nafasi ileile sawa na nomino za Kiswahili asilia au la. Vilevile, kwa kuwa nadharia hii inahusisha sifa za kimofosintakisia, imefaa katika makala hii kuonesha viambishi vya kimofolojia na vile vyenye sifa za kisintakisia

vinavyoonesha upatanisho wa kisarufi. Kwa hiyo, makala hii imeonesha viambishi vya ngeli vya umoja na wingi na vya upatanisho wa kisarufi ili kuonesha mwelekeo wa usarufishaji wa nomino hizo katika Kiswahili.

Nadharia ya pili ni ya Usarufishaji. Nadharia hii ilianzishwa na August W. Schlegel mwaka 1818 katika kitabu chake kilichoonesha wazo la usarufishaji kwa mara ya kwanza. Vilevile, dhana ya usarufishaji iliunganishwa katika Nadharia ya Mabadiliko ya Kisarufi na Antoine Meillet (1912) (Lehman, 2002). Nadharia ya Usarufishaji inahusika na asili na mabadiliko ya maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali (Heine na Kuteva, 2005). Lengo la msingi la Nadharia ya Usarufishaji ni kufafanua namna maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali zinavyojitokeza na kubadilika kwa kipindi fulani pamoja na kueleza kwa nini zimeundwa kwa namna zilivyo (Heine na Kuteva, 2005). Nadharia hii imehusishwa katika makala hii kutokana na masuala mawili ya msingi. Suala la kwanza ni kukamilika na kutokamilika kwa usarufishaji wa maumbo au tungo mbalimbali. Kukamilika au kutokukamilika kwa usarufishaji kunatokana na sababu kwamba mchakato wa usarufishaji ni wa taratibu na una mwelekeo wa kuanzia chini kwenda juu unaofahamika kama usarufishaji wa kidarajia (Lamiroy na De Mulder, 2011). Kutokana na kufanyika taratibu kwa mchakato wa usarufishaji, baadhi ya michakato katika lugha inaweza kudhaniwa kuwa haijakamilika lakini ukweli ukawa michakato hiyo imechelewa kufanyika, hatimaye hukamilika baada ya wakati fulani (Schiffman, 2010) au pengine haikamiliki kabisa (Hakimu, 2020).

Suala la pili ni kuwapo kwa wazo la usarufishaji wa kimvutano. Huu ni mchakato wa usarufishaji unaotokana na kuathiriana kwa lugha moja na nyingine (Heine na Kuteva, 2010) ambazo katika muktadha wa makala hii ni Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu. Heine na Kuteva (2010) wanataja aina mbili za usarufishaji wa kimvutano ambazo ni usarufishaji wa kawaida na wa kuiga. Usarufishaji wa kawaida unahusu uhamishaji wa dhana za kisarufi kutoka katika lugha kopeshi kwenda lugha pokezi na kuzitumia dhana hizo kwa misingi ya lugha pokezi. Vilevile, usarufishaji wa kuiga ni ule ambao dhana na utaratibu wake huhamishwa kutoka lugha kopeshi kwenda lugha pokezi. Usarufishaji huu unatofautiana na usarufishaji wa kawaida kwa sababu lugha pokezi huchukua neno pamoja na mbinu zake za kiisimu za kulitumia kutoka katika lugha kopeshi. Kwa hiyo, matumizi ya nadharia hii yamesaidia kubaini iwapo nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu zimesarufishwa katika lugha ya Kiswahili kiukamilifu au la kwa kufuata utaratibu wa lugha pokezi (usarufishaji wa kawaida) au utaratibu wa lugha kopeshi (usarufishaji wa kuiga). Hatimaye, mwelekeo wa usarufishaji ulio chanya na hasi katika nomino za Kiswahili zilizokopwa kutoka lugha ya Kiingereza na Kiarabu umetambuliwa.

## 5.0 Mwelekeo wa Usarufishaji wa Nomino za Kiswahili zenye Asili ya Kiingereza na Kiarabu

Mwelekeo wa usarufishaji ni hali inayoonesha maneno yalivyojipatia sifa za kisarufi au yanavyobeba viambishi mbalimbali kiukamilifu au la. Ukamilifu huo wa usarufishaji ndio unaobeba dhana ya uchanya au uhasi wa usarufishaji. Msingi wa ubainishaji wa usarufishaji uliokamilika au la unatokana na namna lugha pokezi, yaani Kiswahili inavyotumia viambishi mbalimbali katika maneno yake asilia na namna viambishi hivyo vinavyotumika katika maneno yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Kwa hiyo, kutokana uchanganuzi na ufafanuzi wa data za makala hii, tunapata mielekeo chanya na hasi ya usarufishaji. Mielekeo hiyo imefafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

### 5.1 Mwelekeo Chanya wa Usarufishaji wa Nomino za Kiswahili zenye Asili ya Kiingereza na Kiarabu

Kutokana na data za makala hii, umebainika mwelekeo chanya wa usarufishaji kutokana na namna nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu zinavyobeba viambishi vya ngeli kwa ukamilifu sawa na nomino zingine za Kiswahili asilia. Nomino hizo zimebeba viambishi vya umoja na wingi kabla ya mzizi kama zilivyo nomino zingine za Kiswahili asilia kama ilivyooneshwa na Mgullu (2012) katika ngeli ya {m-mi} kwenye maneno *m-ti* (mti) - *mi-ti* (miti) na *m-kono* (mkono) - *mi-kono* (mikono). Vilevile, nomino hizo zina uwezo wa kubeba viambishi vya upatanisho wa kisarufi vinavyoonesha uhusiano wa maneno katika sentensi ili kuleta muundo na maana inayokubalika. Viambishi hivyo vya umoja na wingi na vya upatanisho wa kisarufi vimeoneshwa kwa kuzingatia Nadharia ya Mofolojia ya Ongezeko la Maneno kwa kuzingatia nafasi za viambishi hivyo. Ubebaji wa viambishi hivyo umedhihirisha usarufishaji wa kawaida kwa sababu nomino za Kiingereza na Kiarabu zinatumiwa katika Kiswahili kwa kubeba viambishi vya ngeli za Kiswahili asilia. Maneno *box* na *ajab* ya Kiingereza na Kiarabu mtawalia, kwa mfano, wingi wake ni *boxes* na *a`a`jāb* (اعجاب). Maneno hayo yameingia katika ngeli za {ji/Ø - ma} kwa neno *boksi* na {Ø-ma} kwa neno *ajabu* na kuchukua upatanisho wa {li-ya} na {i-ya} mtawalia kama inavyoonekana katika mfano Na. 1 hapa chini:

1. Umoja Wingi	Upatanisho wa kisarufi	
boksi ma-boksi	Boksi limejaa nazi	<b>Maboksi yamejaa nazi</b>
ajabu ma-ajabu	Ajabu imetokea	<b>Maajabu yametokea</b>

**Chanzo:** Data ya Maktabani (2023)

Mfano namba 1 unadhihirisha kuwa usarufishaji wa kawaida na uliokamilika kutokana na maneno hayo kuchukua viambishi vya wingi vya ngeli husika. Pia, mfano huo unaonesha kuwa maneno hayana viambishi vya umoja lakini kiuhalisi ngeli hizi umoja wake unaweza kuwa na kiambishi au kapa (Ø) katika baadhi ya

maneno ya Kiswahili asilia kama ilivyo katika neno *tunda - ma-tunda*. Kwa hiyo, mfano huu unaonesha usarufishaji chanya kwa kuwa nomino hizo zimesarufishwa kwa kuwa na viambishi vya wingi vilivyochukua nafasi ileile kama nomino za Kiswahili asilia.

Kwa hiyo, imethibitika kuwa baadhi ya nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu zinabeba viambishi vya umoja na wingi na vile vya upatanisho kama zilivyo nomino za Kiswahili asilia kama ilivyooneshwa na Mgullu (2012). Hii inatokana na kwamba, kama ilivyo kwa nomino za Kiswahili asilia, matumizi ya viambishi hivyo yanasaidia kubainisha hali ya nomino katika miktadha mbalimbali. Viambishi vya upatanisho wa kisarufi, kwa mfano, vinasaidia kuonesha umoja au wingi wa nomino isiyokuwa na viambishi hivyo kimofolojia katika muktadha wa sentensi. Hii ni kwa sababu sio rahisi kuitambua kama ipo katika umoja au wingi bila kuiingiza katika muktadha wa sentensi. Kwa mfano, nomino *chaja* na *dakika* za Kiingereza na Kiarabu mtawalia, zinatambulika kuwa zipo katika umoja au wingi katika muktadha wa sentensi kama inavyoonekana katika mifano Na. 2 na 3 ifuatayo:

2. (a) Chaja ya simu imeletwa.  
(b) Chaja za simu zimeletwa.
3. (a) Dakika imepita.  
(b) Dakika zimepita.

**Chanzo:** Data ya Maktabani

Mifano Na. 2 na 3 inaonesha viambishi vya upatanisho {i-/zi-} kuwa ndivyo vinavyoitambulisha nomino husika kama ipo katika umoja au wingi kama ilivyo kwa baadhi ya nomino za Kiswahili asilia zisizokuwa na umbo la umoja na wingi. Hali hii inaonesha mwelekeo wa usarufishaji chanya kwa sababu nomino hizo zinaendana na baadhi ya nomino za Kiswahili asilia katika ubebaji wa viambishi kimofolojia na kisintaksia.

Pamoja na hayo, baadhi ya viambishi vya ngeli vya umoja na wingi vinafanana na kutofautiana na baadhi ya vile vinavyoonesha upatanisho wa kisarufi. Ngeli ya {ki-/vi-} kwa mfano, viambishi vya ngeli vya umoja na wingi vinafanana na vile na vya upatanisho wa kisarufi katika tungo. Hii ni tofauti kwa ngeli ya {ji-/ma-/Ø} ambayo vipatanishi vyake ni {li/ya}. Kwa hiyo, kutokana na hali ya kufanana na kutofautiana kwa viambishi vya ngeli na vile vya upatanisho, imekuwa muhimu kuvihusisha vyote katika makala hii. Mifano Na. 4(a) na 5(b) inaonesha nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu zinazolingia katika ngeli za {m-/mi-} na {ji-/ma-/Ø} na upatanisho wake {u-i} na {li-/ya-} mtawalia ambavyo havifanani. Tazama mifano ifuatayo kwa ufafanuzi zaidi:

4. Ngeli ya {m-/mi-} na upatanishi wa {u-/i-}



- (a) **Mk**kakao umeoteshwa  
 (b) **Mi**kakao imeoteshwa

Ngeli ya {ji-/ma-/Ø} na upatanisho wa {li-/ya-}

- (a) Kochi **li**menunuliwa  
 (b) **Ma**kochi **ya**menunuliwa

**Chanzo:** Data za Maktabani

Mifano Na. 4 na 5 inaonesha namna viambishi vya umoja na wingi vinavyotofautiana na vile vya upatanisho wa kisarufi. Kwa ujumla, matumizi ya viambishi vya ngeli (vya umoja na wingi) sambamba na vile vya upatanisho wa kisarufi yamesaidia kuonesha msambao na nafasi ya nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu katika ngeli hizo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 linalofuata.

**Jedwali Na. 1: Msambao wa Nomino za Kiingereza na Kiarabu katika Ngeli za Nomino**

Ngeli zenye Viambishi Awali Viwili vya Umoja na Wingi				
Ngeli		Nomino zenye Viambishi vya Umoja na Wingi	Asili ya Neno	Sentensi zenye Viambishi vya Upatanisho wa Kisarufi
Viambishi vya Umoja na Wingi	Viambishi vya Upatanisho			
Mu/m/mw-wa	a-wa	mpagani-wapagani	Kiingereza	Mpagani anaabudu wapi? Wapagani wanaabudu wapi?
m-mi	u-i	mkalatusi-mkalatusi	Kiingereza	Mkalatusi umekatwa Mikalatusi imekatwa
Ji/ Ø –ma	li-ya	kochi-makochi	Kiingereza	Kochi limenunuliwa Makochi yamenunuliwa
Ki-vi	Ki-vi	kibali-vibali	Kiarabu	Kibali kimeshapatikana Vibali vimeshapatikana
u-N/Ø	u-zi	ubeti-beti	Kiarabu	Ubeti umeandikwa Beti zimeandikwa
u-ma	u-/ya-			
Ngeli zenye Kiambishi Awali cha Umoja tu pamoja na Mofu Kapa ya Kiambishi cha Wingi				
Ngeli		Nomino	Asili ya Neno	Sentensi
u-Ø	-u	Uanadamu	Kiarabu	Uanadamu uwepo
Ngeli zenye Kiambishi Awali cha Wingi tu Kapa cha Umoja				
Ngeli		Nomino	Asili ya Neno	Sentensi
Ø-ma	i/li-ya	bomu-mabomu	Kiingereza	Bomu limelipuka Mabomu yamelipuka
Ngeli za Nomino zisizo na Kiambishi Awali chochote				
Ngeli		Nomino	Asili ya Neno	Sentensi
Ø-Ø au N-	i-zi	Advansi	Kiingereza	Advansi imeshalipwa

Ngeli zenye Viambishi Awali Viwili vya Umoja na Wingi				
/N-				Advansi zimeshalipwa
Ku <sup>2</sup>		Kutubu	Kiarabu	Kutubu dhambi kuna faida
Pa/ku/mu				

**Chanzo:** Data ya Maktabani (2023)

Vilevile, msambao wa nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu unaonesha kuwa kuna ngeli zilizojipatia nomino kama vile {mu-/wa-, m-/mi-, ki-/vi-, u-N/Ø, u-/ma-, u-/Ø, Ø-/ma- na ku-} ilhali chache hazina, mathalani {u-/ma- na pa-/ku-/mu-}. Hali hii inadhihirisha mwelekeo chanya kwa ngeli zenye nomino na mwelekeo hasi kwa zile ambazo hazina. Hata hivyo, msambao huu una ughairi katika ngeli ya {N/Ø-N/Ø} pamoja na kwamba ngeli hiyo ina nomino za Kiingereza na Kiarabu. Ughairi huo unaonesha mwelekeo hasi wa usarufishaji ambao umefafanuliwa katika sehemu inayofuata. Hata hivyo, mwelekeo hasi haukuoneshwa katika makala hii kwa kigezo cha msambao tu, bali katika ngeli zilizojipatia nomino za Kiingereza na Kiarabu kiughairi.

## 5.2 Mwelekeo Hasi wa Usarufishaji wa Nomino za Kiswahili zenye Asili ya Kiingereza na Kiarabu

Mwelekeo hasi wa usarufishaji umedhihirika katika nomino za Kiingereza na Kiarabu kwa namna mbili zinazofafanuliwa kama ifuatavyo: mosi, maneno mengi kuangukia katika ngeli ya {N/ Ø -N/ Ø -} isiyokuwa na viambishi vya umoja na wingi kama ilivyooneshwa na Mgullu (2012) na Mdee (2014). Nomino hizi hupata viambishi vya upatanisho wa kisarufi ambavyo ni {i-/zi-}. Viambishi vya upatanisho vinajitokeza katika muundo wa sentensi pale ambapo nomino za ngeli hii zitatumika katika muktadha wa sentensi. Baadhi ya mifano ya nomino hizo ni kama *albamu*, *chaja*, *kilometa* (Kiingereza), *saa*, *taa*, *adhabu* (Kiarabu). Kwa hiyo, nomino ya Kiingereza au Kiarabu isipopata viambishi vya umoja na wingi huingia katika ngeli hii. Hata hivyo, jambo la kuzingatia ni kwamba baadhi ya nomino za Kiingereza na Kiarabu zinazokosa viambishi vya umoja na wingi katika Kiswahili, zina viambishi vya umoja na wingi katika lugha zilikokopwa. Hii ina maana kwamba umbo lililoko katika umoja linatofautiana na la wingi wake. Tuzingatie mifano ya nomino zifuatazo katika mfano Na. 6:

6. <i>albamu</i>	<i>albam-albams</i> (Kiingereza)
<i>balbu</i>	<i>bulb-bulbs</i> (Kiingereza)
<i>bajeti</i>	<i>budget-budgets</i> (Kiingereza)
<i>nafsi</i>	<i>nafs-nufūs/anfūs</i> (Kiarabu)
<i>dakika</i>	<i>daqiiqa-daqaa`iq</i> (Kiarabu)

<sup>2</sup> Kwa kuwa hakuna nomino iliyoingizwa kama kidahizo kwenye kamusi zilizopitiwa ikiwa na kiambishi {ku-}, mwandishi wa makala ametumia kiambishi hicho kuonesha matumizi yake katika baadhi ya nomino za Kiingereza na Kiarabu zinazopatikana katika kamusi hizo.

Nomino za Kiingereza na Kiarabu katika mfano Na. 6 zinaonekana kuwa na umoja na wingi unaotofautiana kutokana na viambishi vya wingi katika nomino hizo. Hii inaonesha kuwa nomino hizo zimesarufishwa katika Kiswahili bila viambishi vya wingi baada ya kukopwa. Umoja na wingi wa nomino hizo unajulikana kutokana na matumizi yake katika sentensi. Pamoja na hayo, zipo nomino nyingi za Kiswahili asilia zinazoangukia katika ngeli hii ambayo nayo umoja na wingi wake unajulikana katika muktadha wa sentensi. Mifano ya maneno hayo ni *nyumba*, *nyama*, *nyasi*, *ngoma*, *ndizi*, *mboga*, *nyota* na *nyanya*. Hata hivyo, tofauti ya nomino hizi na zile za Kiingereza na Kiarabu ni kwamba, baadhi ya nomino za Kiswahili asilia huanza na nazali /n/ au /m/. Nomino za Kiingereza na Kiarabu zinazoangukia katika ngeli hii si lazima zianze na nazali /n/ bali huweza kuanza na konsonanti zingine kama katika nomino *chenji*, *dakika*, *koki*, *taa* na *saa* na zingine. Sambamba na hayo, zipo nomino chache za Kiswahili zinazokiuka kanuni kwa kutokuanza na sauti ya nazali kama zilivyo nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Mifano ya nomino hizo ni *chupa* na *chupi*. Pengine nomino hizo zinahitaji kuchunguzwa zaidi asili yake ili kuthibitisha ughairi wake kwa sababu kamusi zilizopitiwa zinaonesha kuwa za Kiswahili asilia. Hali ya nomino za Kiingereza na Kiarabu kutokufuata utaratibu wa nomino asilia imedhihirisha mwelekeo hasi wa usarufishaji. Usarufishaji wa namna hii unatokana na sababu kwamba maneno ya namna hii hayaingii katika aina za usarufishaji zilizobainishwa na Heine na Kuteva (2010), yaani usarufishaji wa kawaida au wa kuiga. Hii ni kwa sababu nomino hizo hazikupata sifa sawa na nomino za Kiswahili asilia zinazoingia katika ngeli hiyo na wala kubaki na sifa zake asilia za lugha zilikokopwa. Kama uhalisia wa data ulivyo, hali hii inadhihirisha usarufishaji usiokamilika kutokana na sababu hizo.

Pili, kuwapo kwa ngeli za majina ambazo hazikupata maneno ya Kiingereza na Kiarabu. Kutokana na ngeli zilizowasilishwa katika Jedwali Na. 1, ngeli ya {u-/ma-} yenye vipatanishi vya kisarufi {u-/ya-} haikupata nomino za Kiingereza wala Kiarabu. Hata hivyo, baadhi ya ngeli katika Jedwali Na. 1 zikitazamwa kwa haraka zinaweza kufikiriwa kuwa zinachukua kiambishi {u-} cha ngeli hii, ila tofauti ni kwamba ngeli hizi zinapata viambishi tofauti katika wingi na katika viambishi vya upatanisho. Katika nomino za Kiswahili asilia, ngeli hii inachukua nomino kama *ugonjwa-magonjwa* na *uovu-maovu*. Kwa hiyo, kitendo cha ngeli hii kukosa maneno ya Kiingereza na Kiarabu kinadhihirisha kuwapo kwa mwelekeo hasi wa usarufishaji kutokana na ngeli hiyo kukosa maneno yenye asili ya lugha hizo. Pia, inafikiriwa kuwa kwa kuwa usarufishaji hufanyika taratibu na kidarajia, inawezekana mchakato wake unaendelea, umeshapita au hautakamilika (Hakimu, 2020). Hii inatokana na sababu kwamba inawezekana kuna hali ya msambao wa ngeli katika nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu usio sahihi kutokana na baadhi ya majina kuangukia katika ngeli isiyoendana nayo kwa mujibu wa sifa za ngeli husika. Usahihi wa msambao wa nomino katika ngeli ni suala ambalo linaweza kutafitiwa

zaidi. Hii ni kwa sababu, pengine msambao wa nomino hizo katika ngeli ni suala la kinasibu; matumizi halisi ya nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu katika miktadha mbalimbali ndio yanayoukilia nomino hiyo kuangukia katika ngeli fulani.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii inahusu mwelekeo wa usarufishaji wa nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Mielekeo chanya na hasi ya nomino imeoneshwa katika makala hii. Mwelekeo chanya wa usarufishaji wa nomino za Kiingereza na Kiarabu umetokana na uwezo wa baadhi ya nomino hizo kubeba viambishi vya umoja na wingi pamoja na vile vya upatanisho sawa na nomino za Kiswahili asilia. Pia, usarufishaji hasi umejitokeza katika nomino ambazo zimekuwa na utofauti katika kuingia kwake katika ngeli za nomino kutokana na kuwa na sifa zisizoendana na zile za ngeli husika. Vilevile, usarufishaji hasi umejitokeza kutokana na baadhi ya ngeli kukosa nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu zilizoingia humo. Hivyo, usahihi wa msambao wa nomino katika ngeli za Kiswahili unaweza kuchunguzwa zaidi. Kwa ujumla, usarufishaji wa nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu katika Kiswahili umedhihirika kwa kuzingatia Nadharia ya Mofolojia ya Ongezeko la Maneno pamoja na Nadharia ya Usarufishaji. Kwa hiyo, udhihirikaji wa usarufishaji wa nomino za Kiswahili zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu ni jambo la msingi la kuzingatia katika uchambuzi na ufafanuzi wa data za kimofolojia na kimofosintaksia katika Kiswahili. Hili litawasaidia wataalamu na wajifunzaji wa mofolojia ya Kiswahili kufahamu tofauti za udhihirikaji wa nomino za Kiswahili katika ngeli za majina.

## Marejeleo

- BAKITA (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Limited.
- Dzahene-Quarshie, J. (2010). "English in Contact with Swahili: Enrichment or Threat?" *LÉTÜNK*, 4: 55-69. Inapatikana katika [https://www.adattar.vmmi.org/cikkek/1896/letunk\\_2010.04\\_06\\_josephine\\_dzahene\\_quarshie.pdf%OD](https://www.adattar.vmmi.org/cikkek/1896/letunk_2010.04_06_josephine_dzahene_quarshie.pdf%OD). Ilisomwa tarehe 18 Novemba 2023.
- Dzahene-quarshie, J. (2012). "English Loans in Swahili Newspaper Football Language". *Ghana Journal of Linguistics*. 1(1): 35-56.
- Egbe, R.N. na Akpan, I.J. (2016). "The Role of Borrowed Word in Language Development: The Case of Ejagham and English". *LWATI: A Journal of Contemporary Reaserch*. 14(1): 45-58. Inapatikana katika [ajol.info/index.php/lwat/article/view/16053](http://ajol.info/index.php/lwat/article/view/16053). Ilisomwa tarehe 21 Julai 2024.
- Geurts, B. (2000). "Explaining Grammaticalization (the Standard Way)". *Linguistics*. 38(368): 781-788. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1515/ling.2000.006>. Ilisomwa tarehe 5 Desemba 2023.
- Gichuru, T.M. (2020). Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo

- Linganishi wa Kikale na Kisasa. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta. Inapatikana katika [https://ir-library.ku.ac.ke/bitstream/handle/123456789/21358/Mabadiliko ya maana za leksia....pdf?sequence=1&isAllowed=y](https://ir-library.ku.ac.ke/bitstream/handle/123456789/21358/Mabadiliko_ya_maana_za_leksia....pdf?sequence=1&isAllowed=y). Ilisomwa tarehe 10 Desemba 2023.
- Hakimu, J. (2020). Ubantuishaji wa Kimofolojia katika Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Heine, B. na Kuteva, T. (2005). *Language Contact and Grammatical Change*. New York: Cambridge University Press.
- Heine, B. na Kuteva, T. (2010). "Language Contact and Grammaticalization". Katika R. Hickey (Mh.), *The Handbook of Language Contact*. UK: Wiley-Blackwell. Kur. 86-105.
- Ideh, E.A. na Tibetegeza, E.R. (2022). "Attitude of Learners Towards English and Kiswahili in Tanzania". *KIU Journal of Humanities*. 7(1): 59-70. Inapatikana katika [http://www.researchgate.net/publication/367310935\\_attitude\\_of\\_learners\\_towards\\_English\\_and\\_Kiswahili\\_in\\_Tanzania](http://www.researchgate.net/publication/367310935_attitude_of_learners_towards_English_and_Kiswahili_in_Tanzania). Ilisomwa tarehe 22 Julai 2024.
- Katamba, F. (1994). *English Words*. London: Routledge.
- Lamiroy, B. na De Mulder, W. (2011). "Degrees of Grammaticalization Across Languages". Katika B. Heine na H. Narrog (Wah.), *Handbook of Grammaticalization*. Oxford: Oxford University. Kur. 302-318. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1093/oxfordhb/9780199586783.013.0024>. Ilisomwa tarehe 5 Desemba 2023.
- Massamba, D.P.B. (2015). *Historia ya Kiswahili 50KB hadi 1500BK*. Nairobi: JKF.
- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee, J.S. (2014). "A Comparative Analysis of Kiswahili and Echijita Noun Classes". *Huria: Journal of the Open University of Tanzania*. 17: 14-41.
- Mdee, J.S., Njogu, K. na Shafi, A. (2021). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers PLC.
- Mgullu, R.S. (2012). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.
- Mwaliwa, H.C. (2018). "Modern Swahili: The Integration of Arabic Culture into Swahili Literature". *Tydskrif Vir Letterkunde*. 55(2): 120-133. Inapatikana katika <https://doi.org/10.17159/2309-9070/tvl.v.55i2.1631>. Ilisomwa tarehe 20 Novemba 2023.
- Panhwar, I. na Ilyas, R. (2021). "Exploring Reasons on Lexical Borrowing from English Language (L2) to Sindh Language (L1)". *Journal of Literature*,

- Languages and Linguistics*. 83: 22-25. Inapatikana katika Doi:10.7176/JLLL/83-03. Ilisomwa tarehe 21 Julai 2024.
- Polome, E.C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Center for Applied Linguistics.
- Schadeberg, T.C. (2001). "Number in Swahili Grammar". *Swahili Forum*. 68: 7-16.
- Schiffman, H.F. (2010). "Language Contact in South Asia". Katika R. Hickey (Mh.), *The Handbook of Language Contact*. Oxford: Wiley-Blackwell. Kur. 738-756.
- Stump, G.T. (2001). *Inflection Morphology: A Theory of Paradigm Structure*. New York: Cambridge University Press.
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza (Toleo la Pili)*. Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.